SOMO LA 14

MAFUNZO YA BIBLIA KUHUSU MUNGU

“Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma” – Yohana 17:3

MSURURU WA MASOMO YANAYOFUATIA yataangazia ufunuo wa Biblia kumhusu Mungu, Roho Takatifu, Malaika na Yesu Kristo. Kila mojawapo ya mada ni ya lazima na ni muhimu mno, hasa hili somo la kumhusu – MUNGU.

Kwa nini ni muhimu kuwa na ufahamu usio na walakini kuhusu Mungu? Kwanza. twaambiwa ya kuwa wokovu wetu unategemea sisi kufanyika wana wa kiume na wa kike wa Mungu – “… kwa maana sisi ni hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu… Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike” (2 Kor 6: 16 - 18)

- Kwa upande wake inategemea sisi kuyajua yanayomhusu Mungu
- “ Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu haututambui, kwa kuwa haukumtambua yeye” (1 Yohana 3:1)

“Jina lako nimewadhihirishia watu wale ulionipa katika ulimwengu; walikuwa wako, ukanipa mimi, na neno lako wamelishika” (Yohana 17: 6)

Kwa lugha ya maandiko, kudhihirisha jina inamaanisha kueleza kila kitu kuhusu historia, sifa na lengo la yule mwenye lile jina.

Ni wazi kuwa ufahamu wa Mungu ni muhimu. Zaidi ya hili, kumjua Mungu kwapatikana mahali ambapo ameweka maelezo hayo – kwa kuongozwa kwa neno lake. Ni kweli kuwa asili ya vitu vyatoa ushahidi mwafaka kuwa mambo yake yote yamepangwa kwa hekima na ufahamu, na inazingatia sheria za usahihi wa vitu hasa na kawaida yake. Inatilia nguvu mtu mwenye akili nzuri kutambua kuwa Mungu yupo – kuwa lazima kuwe na chanzo kuu ya hekima na nguvu. Hata hivyo, asili ya mambo haituelezi chochote kuhusu Mungu alivyo, sifa zake, kusudi lake, wala mapenzi yake kumhusu mwanadamu. Kwa maelezo hayo muhimu kuna mahali pamoja pa kuyapata hayo – Neno la Mungu, Biblia.

Uvumi wa upofu wa mwanadamu, uliopita na uliopo, watuongoza kwenye ushirikina wa jadi na wa sasa.

Jinsi gani twafaa kuvutiwa, kushukuru na kufurahia kumjua Mungu, ambaye ameumba na kudhibiti ulimwengu katika utukufu na uzuri wa ajabu, alivyokubali kujionyesha kwetu kwa

kutwambia kuhusu kusudi na matarajio yake ya upendo. Inamaanisha amani ya sasa na furaha ya milele siku za usoni.

Yasikitisha ya kuwa, kwa kuangalia somo hili tutagundua ya kwamba mara nyingine mafunzo ya Biblia yanakinzana na yale ya Wakristo wengi. Ingawa maelezo sahihi yanaangaziwa katika Biblia, na ni maridadi katika maelezo rahisi ya kina, na mazuri, yahuzunisha kuona nadharia za kipegani zilizochanganywa na mafundisho mazuri ya mitume zilivyosababisha mkanganyiko na kutia giza kikuu kwa somo hili; na hali hii imewafanya raia wengi pasipo kufikiria na bila kuuliza swali kukubali dhana ya mungu watatu katika mmoja – “Utatu” – (Wayunani wapegani walipitisha msimamo huu) uwe wa Mungu wa Biblia.

Ili tupate kuelewa asili ya mafundisho haya potofu, Encyclopedia Britannica, toleo la 9, kifungu XX –206—XX Theism iliyoandikwa na mtu anayeshikilia Utatu, yanasema “Mapendekezo ya kitengo cha mbinu za utatu yalindwa baada ya jitihada nyingi kipindi cha karne kadha, na yafaa yaelezeke kwa dhana iliyoandaliwa kwa metafizikia ya Wayunani na Warumi. Mageuzi ya mafundisho ya Utatu yalikuwa ya muhimu sana katika historia ya kanisa kwa karne 5. Hatua ya theolojia na falsafa ndiyo iliyokuwa sura tofauti ya Ukristo wa enzi za Kati.”

Haya ndiyo maelezo ya washikilizi wa Utatu wenyewe kuhusu asili ya mafundisho haya. Kwa hivyo theolojia ya asili, ilitokana na falsafa ya Kiyunani ya Plato, yafunza kuwa kuna miungu watatu, au sehemu tatu ya miungu wao wa milele; wote sawa na wa milele, wote wenye nguvu sawa, wote wakijitegemea kuishi; na sehemu hizi zote zikiwa ni kitu kimoja. Wakristo wamechukulia miungu hii tatu inajulikana kama Utatu (jambo ambalo halipatikani katika Biblia)

Mungu baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu; kila mmoja akiwa Mungu hasa, kila mmoja hana mwanzo, kila mmoja akiwa na nguvu sawa, kila mmoja akiwa ametengana na wengine ingawa ni mmoja. ‘ Mkanganyiko wa fundisho hili yajieleza kama isiyofahamika, ‘ isiyoeleweka’ ambao ni ukweli kabisa.

Kinyume na mafunzo haya ya asili, twaona Maandiko yakitilia mkazo Umoja, Mungu Mmoja tu, kama jambo la kimsingi kumhusu – ni kama yatuonya dhidi ya nadharia zenye dhana inayoleta wingi wa Mungu – kama vile Utatu: mwanadamu amekuwa na miungu wengi tangu hapo. Musa alisema – “Sikiza, Ee Israeli; BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja” (Kumbukumbu 6:4). Yesu alipoulizwa amri ya KWANZA kwa zote, aliwaelekeza kwa maneno hayo yenye mwongozo thabiti ya Musa: “Ya kwanza ndiyo hii, Sikia Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja” (Marko 12:29). Paulo pia aliwafunza Wakorintho mambo sawa na haya: “Lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake… yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo” (1 Wakorintho 8:6)

Angalia hasa, kwanza, anasema kuna Mungu mmoja; na kuwa, mbali na huyo Mungu mmoja, kuna Bwana Yesu Kristo. Hii ni wazi kabisa kuwa Yesu si sehemu ya huyo Mungu mkuu. Yesu mwenyewe kila mara anamtaja Mungu kama “Baba”; anamwomba, anasema yeye mwenyewe hawezi kufanya jambo lolote: Anasema na kutenda yale anayoagizwa na kufanywa na yeye.

Paulo anasema tena – “Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote” (Waefeso 4: 6)

“Kwa sababu Mungu ni mmoja na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu” (! Timotheo 2:5)

Angalia tena Paulo anavyotofautisha kwa makini kabisa kati ya “Mungu Mmoja” na “Mwanadamu Kristo Yesu.” Kristo ni mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu. Sio sehemu ya Mungu huyo mmoja. Anazungumziwa kama kitu kiteule na yule Mungu mmoja. Anatajwa, hata wakati huu ambapo ana mwili wa utukufu wa milele, kama “mwanadamu.”

Tena, Mungu mwenyewe twaona katika kitabu cha Isaya akirudia mara kadha ya kuwa yeye ni mmoja hasa, kama tunavyopata katika vifungu hivi:

“Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine; zaidi yangu mimi hapana Mungu” (Isaya 45:5)

“Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho; zaidi yangu mimi hapana Mungu… Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba;mimi sijui mwingine” (Isaya 44: 6 - 8)

Kifungu katika Biblia zetu kinachoonekana kuunga mkono mafundisho haya ya Utatu ni 1 Yohana 5:7. Maneno haya yameingizwa hapa na mwanadamu kwa lengo la kuunga mkono mafundisho hayo maarufu (Mfumo wa “kipengele cha binadamu” ambacho mara kwa mara hupenyeza katika kazi ya utafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine. Kifungu hiki kimetumbukizwa hapa zaidi ya miaka 200 ikijulikana kuwa ni bandia. (lakini wengine bado wanalitumia, wakiwa na matumaini ya kuwa wasikilizaji wao hawatagundua ni cha uongo). Waumini wa Utatu wanaojua ukweli wa jambo hili wanakubali kuwa ni bandia. Hakipatikani popote katika miswada ya Kiyunani ya Biblia kabla ya karne ya 16, na katika miswada minne tu baadaye, miswada isiyo na uzito. Kifungu hiki hakijanukuliwa na waandishi watangulizi kabla ya mwishowa karne ya 5. Haikuwahi kutajwa na yeyote yule kutoka pande zote za suala hili kipindi chote cha mabishano makali kilichovuma karne yote ya 4, ambayo hatimaye Utatu ukaimarishwa kama dini ya dola kwa upanga.

Maandiko yatangaza kuwa vitu vyote vimetokana na Baba (1 Kor. 8:6, 11:16; Warumi 6:30 ; n.k). Hili jina, “Baba” laonyesha yeye ndiye chanzo. Kama chanzo, yeye pia ndiye kituo cha kati. Maandiko yanafunza wazi Mungu ana makao yake maalum (kinyume na falsafa ya dini za wanadamu) ingawa yuko kila mahali kwa roho yake ambayo inaujaza ulimwengu mzima. Paulo anasema, “Amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa” (1 Timotheo 6: 16)

Ikiwa Mungu anakaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa, ni lazima yuko mahali fulani halisi, mahali tofauti pa kipekee ambapo si kila mahali akijidhihirisha kotekote (hata hapa walipo wanadamu) kwa roho yake. Suleimani anasema hivi : “Mungu yuko mbinguni, na wewe uko chini, kwa hivyo maneno yako na yawe machache” (Mhubiri 5:2).

Na Yesu akawaambia wanafunzi waombe hivi : “Baba yetu uliye mbinguni” (Mathayo 6:9)

Daudi katika zaburi pia anaonyesha mahali maalum anapokaa Mungu, kama - “Maana ametazama toka patakatifu pake pa juu, Toka mbinguni BWANA ameangalia nchi” (Zaburi 102:19,20)

“Mbingu ni mbingu za Bwana, bali nchi amewapa wanadamu” (Zaburi 115:16).

Katika maombi aliyoyafanya Suleimani alikariri ukweli huu – “Sikia huko mbinguni, makao yako” (1 Mfalme 8:30)

Maelezo haya yana maana – na yanaweza kueleweka – kwa misingi kuwa Mungu ana makao maalumu mbinguni. Ni vigumu sana kukwepa ushuhuda unaotolewa na vifungu hivi kuwa Mungu ni mtu aliyepo na anakaa “mbingu za mbingu” na sio mahali pengine zaidi.

Tena, mafunzo haya bayana ya Biblia yanakinzana na yale maarufu ya dini za jadi kuhusu Mungu, zinazojaribu kumfanya Mungu awe kanuni tu au nishati iliyotengewa ulimwengu mzima, pasipo na mwili, pasi na makao maalum, “pasi na mwili wala sehemu” kama ‘Creed’ – imani inavyokariri. Lakini hii ni falsafa ya kibinadamu jinsi mwanadamu anavyofikiria yafaa iwe , kuliko ukweli wa mambo ilivyo kama inavyotangazwa na maandiko. Vifungu ambavyo vimetolewa kufikia hapa vinaashiria kinyume kabisa cha mafunzo ya jadi, yalitumiwa kwa njia rahisi na ya kiasili.

Kuna vifungu vingine vya kuonyesha kuwepo hasa kimwili kwa Muumba. kama tutakavyoona. Mungu mwenyewe alijidhihirisha kwa Musa zaidi na vile alivyofanya kwa mwanadamu mwingine yeyote isipokuwa Bwana Yesu, Alisema hivi, Musa alipokazana auone utukufu wake:

“Huwezi kuuona uso wangu, maana mwanadamu hataniona akaishi: BWANA. Akasema, Tazama, hapa pana mahali karibu nami, nawe utasimama juu ya mwamba; kisha itakuwa wakati unapopita utukufu wangu, nitakutia katika ufa wa ule mwamba na kukufunika kwa mkono wangu hata nitakapokuwa nimekwisha kupita; nami nitaondoa mkono wangu, nawe utaniona nyuma yangu, bali uso wangu hautaonekana” (Kutoka 33: 20 - 23)

Twasoma haya kuhusu kujidhihirisha kwake Mungu kwa Musa:

“BWANA akamwambia Musa, waambie wana wa Israeli hivi, Ninyi wenyewe mmeona ya kuwa nimenena nanyi kutoka mbinguni” (Kutoka 20:22)

“Kwake nitanena mdomo kwa mdomo, maana, waziwazi wala si kwa mafumbo, na umbo la BWANA yeye ataliona” (Hesabu 12:8) (Neno “umbo” limetumika kuonesha cha kuonekana kwa macho).

“Naye BWANA akasema na Musa uso kwa uso, kama vile mtu asemavyo na rafiki yake” (Kutoka 33:11)

“Wala hajainuka tena katika Israel nabii kama Musa, ambaye BWANA alimjua uso kwa uso” (Kumbukumbu 34:10)

Ingawa vifungu hivi vyote vinaangazia udhihirisho wa Mungu kupitia kwa malaika, kinachodhihirishwa ni kikuu kuliko kile chombo cha kudhihirishia. Si chochote kama “dhihirisho,” isipokuwa kama ushahidi na uhalisia wa kuwepo wa yule wanayemdhihirisha. Nguvu na uongozi wa tangu hapo wa Muumbaji hutangazwa kila mara.

“Akaaye milele” (Isaya 57:15)

“Mungu wetu ni moto ulao” (Waebrania 12:29)

“Na tangu milele hata milele” (Zaburi 90:2)

“Wewe uliye na macho safi hata usiweze kuangalia uovu” (Habakuku 1:13)

“Yeye Mungu wa milele, BWANA, muumba miisho ya dunia, hazimii wala hachoki, akili zake hazichunguziki” (Isaya 40:28)

“Mataifa yote huwa kama si kitu mbele zake ” (Isaya 40: 17)

Ni mungu pekee aliyepo kwa kujitegemea kwa hali isiyojulikana. Maisha mengine yote, hata yale ya Yesu aliyepata utukufu, ni sehemu tu ya nguvu zake, kama kijito kinachotoa maji yake kutoka kwa chemchemi kuu moja. Tunasoma hivi kumhusu –

“Mfalme wa wafalme, Bwana wa mabwana, ambaye yeye pekee yake hapatikani na mauti” (1 Timotheo 6:15,16)

“Kwa maana NDANI YAKE yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu” (Matendo 17:28)

“Kwa kuwa vitu vyote VYATOKA KWAKE, viko kwa uweza wake, tena vinarejea kwake” (Warumi 11:36)

“Lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake” (1 Wakorintho 8:6).

“Waipeleka roho yako, wanaumbwa (viumbe wote) … Waiondoa pumzi yao, wanakufa, na kuyarudia mavumbi yao” (Zaburi 104: 30, 29)

Theolojia maarufu yafunza ya kuwa Mungu hakuumba vitu vyote kutokana na kitu chochote. Biblia yafunza kuwa vitu vyote vinatokana na Mungu mwenyewe. Kupitia kwa nguvu ya roho yake, kama vile vifungu vilivyotangulia vinavyoonyesha. Roho ya nguvu ya Mungu, ikitoka kwake kwa radhi yake, na kwa mapenzi na uongozi wake, ameendeleza vitu vyote kama vifaa vilivyoumbwa tunavyoviona.

Uchambuzi wa kina unapofanywa juu ya ulimwengu – vifaa vyote vya kuwepo kwetu kila siku na vile vya anga za mbali – ndipo mtu hutambua “vifaa” vyote vipo kwa wingi na hali mbalimbali kwa masharti ya nguvu moja ya asili. Atomu ya kipengele maalum (kulingana na

mwanadamu na ufahamu wake wa sasa) vyaonekana tu kama bloku za ujenzi ambavyo binadamu huviita Protoni, nyutroni, elektoni, n.k ambavyo ndivyo asili ya nguvu za kuchaji. Taswira ya nadharia mpya inatengezwa ukweli mwingine unaoibuka. Wanapotafuta undani, ndipo inavyokuwa tata na isiyo na upeo, ingawa kimsingi nia moja na tena yafanana, hali ya ajabu ya mlingano wa uumbaji na uwepo wadhihirika. Kwa haya yote, wanaendelea kuamini, au kuamini kiutumwa, viliumbwa pasi na kitu, na vitu vyote hivi vinavyoonekana pasi na mwisho vilivyo na ulinganifu wa ajabu pasi na matatizo vimeibuka tu kiholela bila nguvu zozote kutumika, wala mpango au kusudi. Hii ni hali gani ya kutathmini kazi ya sayansi!

Roho ya nguvu ya Mungu ndivyo msingi wa uumbaji na uwepo wa asili na mwanzo wa kila kitu. Katika hali hii, Mungu yupo kila mahali(omnipresent). Kwa hivyo anajua nini kinafanyika sehemu gani ya ulimwengu kila wakati. Kwa neno moja: ni mjua-yote(omniscient) na mwneye nguvu zote (omnipotent). Kwake yeye ambaye kwa rehema zake amejifafanua wazi na kwa utukufu kwa wale ambao wanataka kumjua na kuwa naye milele, tutamwabudu, na kumhudumia kwa kutoa shukrani zetu zote! Baraka ilioje! Uajibikaji mkuu ulioje!

MASWALI YA SOMO LA 14

1. Tumjue nani ili tupate uzima wa milele?
2. Je, kumkiri Mungu na Yesu kwa kinywa kwatosha kumpa mtu wokovu?
3. Ni wapi tunaweza kupata ufahamu kuhusu Mungu na Yesu?
4. Nini kimefanya ufahamu wa Mungu kukanganya akili za watu?
5. Mafundisho maarufu ya kanisa ya kimataifa kuhusu Mungu 3 yaitwaje?
6. Toa kauli 3 ya maandiko inayothibitisha kuna Mungu mmoja tu, na ya kuwa mafundisho ya kanisa ya miungu 3 ni uongo.
7. Je! Mungu anakaa mahali fulani maalum? Ingawa yuko kila mahali?
8. Toa sababu 2 kuthibitisha.
9. Kiti cha enzi cha Mungu kiko wapi?
10. Ni nani amekaa mkono wa kiume wa Mungu?
11. Je, Mungu ana mwili hasa?
12. Thibitisha kwa maandiko.
13. Mungu amejidhihirisha vipi kwa wanadamu?
14. Ni kwa namna gani vitu vyote viliumbwa kupokea nishati?
15. Vitu hivi vyote vimeumbwa kutoka wapi?
16. Mungu amewezaje kuwa kila mahali; na kufahamu kila kitu, kama anakaa mbinguni?
17. Ufahamu kuhusu Mungu na mwanawe Yesu Kristo ina athari gani kwa maisha yetu?